BALOZI wa Pakistan nchini Kenya Jemedari nawale Ahmed Ashraf akihutubia hafla maalum kua dhimisha siku ya Kiislamu ya "Husein Day" katika msikiti wa Sakina iliyo tayarishwa na jumuiya ya Waislam Mombasa.

TUSISTIZE UDUNGU MAPENZI, UMOJA NA AMANI KATI YA WAISLAMU WOTE

NA ABIDU ZAMAN

AMMAL-HAKIKA hasikitishwa sana kuona kuwa undugu katika uislamu waanza kutoweka, na jambo hili lasababisha na kutolewana lugha, sisi kwa sisi Waislamu.

Mtume Mohammed S.A.W. alipotowa kilma cha "Inna Maal Muslimuna Ikhwan", alitaka sisi Waislamu tunufaike, na kufuata mwendo wake wa kupendana pamoja na kuwa na umoja wa kusaidiyana katika shida yoyote itakayo mkabili muislamu.

Nimasikitiko makubwa leo ukimuona muislamu ahamkimbia au kuchukia mwenziwe. Ikiwa tu Waislamu wa kweli twatakiwa na mwenyezmungu tuwe kitu kimoja na tuondowe utengano tulionao sasa.

Pili haina maana yoyote kwa Muislamu kumkashifu Muislamu mwenziwe. Dini yetu imetuamrisha tuwe wadhibitifu wa siri au aibu ya Muislamu kwa Islamu mwenzake.

Leo sisi twaona fakhri kumkejeli mwenzetu mbele ya jinsi tofauti, ambapo wampa nguvu asokuwa mwislamu kuzidi kuidharau dini yetu. Hebu zingatia kama wewe ukitolewa aibu ambayo hunayo utajisikiaje ndani ya moyo wako.

Kitu amabacho nicha kurudishi nyuma sana na chenye ufisadi wa dini, nikuwa siku hizi kumezuka mtindo wa kukashifiana Waislamu kwa njia ya kueneza makaratasi yasiyo na kichwa wala miguu. Na haya aghalabu hufanzwa na viongozi wa dini.

Ndugu waislamu hebu hatarudi nyuma tuzingatie haya mambo tufanzayo ni maendeleo au ni maangamivu? Tukiwa na mtindo kama huu naona kutakosekana maendeleo na mafanikiyo katika dini yetu.

Yataka tufahamu sisi Waislamu wa sasa tumeipata dini ukiwa imeshakamilika. Hebu kama nikweli tusomeni tarehe za ndugu zetu Waislamu waliopita, tutaona vipi walipata taabu katika kuisimamisha dini. Tusiwe tutaifanza dini kama chombo cha kukashifiana.

Mtu akiwa amepitwa kwa daraja ya elimu asiwe atakuwa ni mwenye wivu. Kitu cha kufanza niajitahidi ili naye awe kama yule aliyempita "Manijtahada Wajada", mwenye kujitahidi hupata.

Tusiwe nyuma katika kutafuta elimu ya dini na ya dunia.

Nimeandika makala haya huku nikidondokwa na machozi ya udungu, tutakwenda sema nini kesho akhera? Tumeandalia zawadi gani huko twendako? Ikiwa zile amali tuzitumazo twazimaliza hapa hapa bila ya kufikiri.

Inshaallah kwa haya machache nadhamu yatatufaa pamoja na kuzinduwa ili kujirekebisha, na kuwa na Imani thabiti katika dina pamoja na kumpenda mtume Mohammed S.A.W. na Waislamu wote.

Wassalamu alikum warahmatullah taala wa barakaat.

Wachezaji wa Libati Heroes, Majengo ambao walishiriki katika ligi ya 4 Mombasa mwaka huu.

Mchezaji wa Klabu ya Black Panther kibwaju bwajuma (kushoto) alipotembelewa na mweka hazina wa Klabu hiyo Mohamed Hassan (Kulia) akiuguza mguu wake hospitalini.

PICHA: ABDU LRAHMAN SHERIFF.

GALGALO ATEKELEZA AGIZO LA KANU

Na Abdulrahman Sheriff

MKUU WA MKOA PWANI, Bw. Luka Galgalo aliahidi na kuhakikisha kuwa hatakubali kumsaidia mwanasiasa yoyote wakati wa uchaguzi wa Kanu utakapotangazwa na Mtukufu Rais Daniel arap Moi na akawaomba wananchi wa Pwani watanye mambo ya maendeleo na kuacha kutusiana hasa nyakati za kampeni ya uchaguzi wa chama kinachotawala nchini. Bw. Galgalo alitoa hakikisho na ombi hilo baada ya kusoma hotuba rasmi ya Rais Moi ya kuadhimisha sikukuu ya Jamhuri Dei katika uwanja wa Manispaa ya Mombasa ambapo halaiki ya wananchi walihudhuria tamasha hilo.

Alitangaza kwamba vitabu vya risiti za Kanu vilikuwa vimeshatambazwa katika kila wilaya mkoani Pwani.

Vitabu hivyo vya risiti za Kanu zitaanza kuuzwa toka Desemba 14 kama agizo la Rais Moi lilivyosema katika hotuba yake ya kuadhimisha Jamhuri Dei na hakuna mwananchi yoyote atakayezuiliwa kununua risiti hizo kwani tunataka kila Mkenya tykiwemo sisi watanyakazi wa Serikali tunahitajika kuwa wanachama wa Kanu, akasema Mkuu huyo wa mkoa wa Pwani.

Bw. Galgalo aliahidi kuwa hatakuwa tayari kumsaidia mgombea uchaguzi yoyote na akahakikisha kuwa haki itatumika kila mahali Pwani kuona viongozi wale wanatakikana na wananchi wenyewe ndio watakaotambuliwa na kutangazwa kama washindi.

Tunatarajia Pwani nzima uchaguzi wa Kanu utakapowadia utamalizika kwa njia za kutana na nawaomba wananchi wadumishe amani wakati huo", akaongeza.

Aliwasitu wananchi wa Pwani kwa kujishirikisha kikamilifu kwenye Harambee na akasema, tumegeuza mwenendo wetu wa hapo awali ambapo watu wa Pwani tulikuwa tukitahamika kama tusopenda kushiriki kwenye mipango hiyo lakini mambo yameanza kubadilika na natarajia tutafanya mengi zaidi siku za usoni".

Aliwashauri wanasiasa na wananchi wasiache mambo ya maendeleo kwa ajili ya uchaguzi na akawasisitiza wasivunjike moyo kuhusu shida ya uchumi.

Si jambo la busara kwetu kuwalaumu viongozi kila kunapotokea matatizo kwani Serikali na viongozi wanajaribu kila wawezalo kuona wananchi wanapata mambo mazuri", akasema Bw. Galgalo.

Kuhusu mchele, Bw. Galgalo alitoa amri kwamba tokea sasa hakuna mwenye duka atakayetakikana kupata pamiti ya kunua mchele kutoka bodi ya Taifa ya Nafaka kwani alisema, "hakuna tena shida ya bidhaa hiyo na kwa hivyo kila mfanya biashara ama mwenye duka anaweza kwenda kujinunulia mchele tani atakazo lakini ahakikishe mchele huo unawafikia wananchi na wala hautanyiwi madhambi yoyote".

Kwenye sherehe hiyo hiyo, Mwenyekiti wa Kanu wilayani Bw. Sheriff Nassir aliwaomba wananchi watanye bidii katika harakati za mipango ya maendeleo na akawahakikisha kuwa kushinda uchaguzi ni yale matendo mazuri mgombea atakuwa ameyatanya hapo mbeleni".

Bw. Nassir, aliye pia Mbunge wa Mombasa ya Kati na Waziri Mdogo wa Leba alisema matendo ya mgombea uchaguzi ndiyo yatakayompatia kura na akawashauri wananchi wajiandikishe kwa wingi kuwa wanachama wa Kanu wakati risiti za chama zitakapoanza kuuzwa.

Naye Mbunge wa Mombasa Kaskazini, Bw. Said Hemed alilaumu vikali tabia ya baadhi ya wakuu fulani wa makampuni ya kuagiza watu kutoka nje ya mkoa hali wananchi wengi wanaoishi Mombasa hawana makazi. Alisema tabia hiyo ni lazima ikomeshwe kwani ni ubora wasio na kazi mjini Mombasa wapate nafasi za kwanza za kuajiriwa na akaongeza, makabila kadha ya nchini Kenya yana raia wanaoishi kisiwani na kwa hivyo wapatiwe nafasi za kwanza ili kupunguza shida ya ukosefu wa kazi".

Mbunge wa Mombasa Kusini, Bw. Abdallah Ndovu Mwidau aliwasihi wananchi wawe na umoja na kupendana ili uthabiti wa nchi uzidi kuimarika kwani alisema, "uthabiti ni jambo la maana kwa nchi yoyote kutanya maendeleo ya kutosha na ndio maana uthabiti wetu Kenya umetutanya tuwe na haki ya kuwachagua viongozi tunaowataka".

Mbunge Maalum, Bw. Omar Bwana pia aligusia mwenendo wa baadhi ya waajiri ya kuwapa makazi watu wa kabila lake ama jamaa zake.

"Wengine huagiza ndugu zao wanaolima na kuwaachisha kulima na kuwapa kazi ambazo zingeliwafaa watu wengine", akatoka Bw. Omar Bwana.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bw. Luka Galgalo aliyesoma hotuba ya Rais katika sherehe za Jamhuri.

PICHA: NATIONAL STUDIO

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

KWENDA KULIA:

1. United Kingdom
3. Moyo
8. Sehemu ya mnyama
10. Nchi Arabuni
11. Langalie
12. Mahali penye maji mengi baharini
13. Nguvu za Mungu
18. Wazimu
21. Hutengeza bara bara
23. Uadilifu
24. Nafasi, sehemu ya ardhi
25. Zuia vita
26. Atatunga ndoa
27. Tamko la kukataa.

KWENDA CHINI:

1. Ukoa haigeuki
2. Mtoto wa ndege
4. Uchatu
5. Sikukuu ya Kiislamu
6. Silaha za kutatunia
7. Sikwamba hana
8. Mwiko zaidi ya mmoja
9. Aeu kama ilivyo
14. Bembeleza
15. Shirika, Mkao
16. Wenyeji wa nchi
17. Taka kitu kimombo
18. Cha kujiangalia
19. Kiungo cha maneno
20. Azidi kimo
21. Tunza mtoto
22. Ota, chipuza.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 152

1. Ali Bakari Sanduku La Posta 86922 Mombasa.
2. P. W. Mpwipniro Sanduku la Posta 90404 Mombasa.
3. Jimmie Munene Sanduku La Posta 87310 Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO 152 —

KWENDA KULIA:

1. KUNGU, 6. KAZA, 7. NAAM, 10. ADAI, 11. ANAO, 12. SH, 13. BA, 14. HIMU, 16. TAIB, 18. JA, 19. OA, 20. TUMA, 23. BOSS, 25. AZOA, 26. ISHA, 27. UBALE.

KWENDA CHINI:

1. KADHI, 2. UZA, 3. NAIBU, 4. UNA, 5. KAA, 6. KASHATA, 8. ANGA, 9. MOMBASA, 15. MUMO, 16. TABIA, 17. IOSHE, 21. UZI, 22. AAU, 24. OSL.



SWAHILI CROSSWORD NO 153

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-Shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za Fimbo hili lipelekwe kwa: *Muhariri COASTWEEK, Sanduku La Posta 87270 Mombasa, Kenya.*
Siku ya Jumatano tarehe December 29, 1982, saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.